KKKT - DKK - JIMBO LA MASHARIKI
LUPILA
USHARIKA WA NKWENZULU
S.L.P. 112
NJOMBE - MAKETE
TAR 17/9/2023

MPENDWA MICHAEL
UJERUMAN

Salam za heri na baraka zikufikie mpendwa wetu katika BWANA tunashukuru ni M-zima na BWANA anazidi kukupigania hapo ulipo kwani neema na Baraka zake zipo juu yako katika kumtumikia Mungu wa mbinguni aliye juu.

Dhumuni la kuandika barua hii kwa ujumla ni kutaka kukujulia hali na kukujulisha kwamba sisi huku kama Kanisa ni wazima na tunaendelea vizuri na kazi na Mungu wetu anazidi kutupigania usiku na Mchana tunaishi na tuko salama pia tunazidi kushukuru kwa msaada wote unaozidi kutoa kwa watoto wetu wote wanaosoma kwani jambo hili limeleta baraka kubwa sana katika masomo yao Mungu akubariki.

Pia mpendwa tunashukuru kwa ajili ya mtoto Jonfesi, Fanueli Huseni Ibrahimu waliopata Meza, Solar kitanda kwani ni msaada ambao umesaidia watoto hawa kuwa na hali nzuri sana ubarikiwe sana Mtumishi wa Mungu.

Jambo lingine tunashukuru kwa ajili ya kutuombea kwa tunaendelea vizuri na hali ya hewa ni nzuri kabisa na tunaendelea na kazi zote salama na pia ni muda wa kupanda mahindi Ngano na Maharage tunashukuru mno kwa kazi yako nzuri ilio njema sana

Mpendwa Mungu azidi kuwabariki sana pale mlipo punguza akawaongezee sana mzidi kuwa na hekima na busara kati ka kumtumikia Bwana. Niandike neno katika Zab 23:1-2 AMEN!

SAHIHI YA MCHUNGAJI [signature]

CamScanner